**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 27/10/2022 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA SOKO KUU LA CHIFU KINGALU.**

**Wajumbe waliohudhuria**:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pascal M. Kihanga | __ | Mstahiki Meya – Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Ally H.Machela | __ | Mkurugenzi wa Manispaa -Katibu |
| 3. | Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele | __ | Naibu Meya - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Emmy Kiula Rajabu | __ | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | __ | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Warda Omari Bazia | __ | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salima Bonzo Mbandu | __ | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Melchior Peter Mwamnyanyi | __ | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Juma Issa Kiduka | __ | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Selestini Savini Mbilinyi | __ | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani | __ | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu | __ | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Hassan Madadi Maringo | __ | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Mwanaidi Ebrahim Ngulungu | __ | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Amina Hussein Zihuye | __ | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Samuel Alfred Msuya | __ | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Joel Albert Kisome | __ | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Rahma Lashayo Maumba | __ | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Latifa Said Ganzeli | __ | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Hamisi Ally Kilongo | __ | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Salum Mrisho Chunga | __ | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Amini Abdallah Tunda | __ | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Aisha Ahmad Kitime | __ | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Lt.Col(Mst) Ahmed S. Mazora | __ | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Eng. Hamisi Hamadi Ndwata | __ | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Athumani Omary Lujuo | __ | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Peter Joel Dhahabu | __ | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Mch. Thomas Benedict Butabile | __ | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Rashid Ramadhani Matessa | __ | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Grace Luwis Mkumbae | __ | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Zuberi George Mkalaboko | __ | Mjumbe |
| 32. | Mhe. Marco Mathias Kanga | __ | Mjumbe |
| 33. | Mhe. Zinduna Kombo Selemani | __ | Mjumbe |
| 34. | Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah | __ | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35. | Mhe. Namala Johaness Mchunguzi | __ | Mjumbe |
| 36. | Mhe. Seif Zahoro Chomoka | __ | Mjumbe |
| 37. | Mhe. Hadija Kombo Kibati | __ | Mjumbe |
| 38. | Mhe. Madaraka S. Bindyanguze | __ | Mjumbe |
| 39. | Mhe. Abdallah Ally Meya | __ | Mjumbe |

**Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb) | __ | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Norah Mzeru (Mb) | __ | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma ( Mb) | __ | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu | __ | Mjumbe |

**Viongozi waalikwa:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Adv. Albert G. Msando | __ | Mkuu wa Wilaya ya Morogoro |
| 2. | Dkt. Mussa Ali Mussa | __ | Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro |
| 3. | Ndg. Neema M. Dachi | __ | Katibu Tawala Msaidizi Mkoa, Huduma za Serikali za Mitaa |
| 4. | Ndg. Ruth John | __ | Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro |
| 5. | Eng. Lacha M. Hafidhi | __ | Kaimu Mkurugenzi wa MORUWASA Morogoro |
| 6. | Ndg. James M. Hiza | __ | TANROADS |
| 7. | Ndg. Adam Abdulla | __ | Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Morogoro |
| 8. | Ndg. Haji Mohamed | __ | Kaimu Afisa Usalma Wilaya |
| 9. | Mhe. Fikiri H. Juma | __ | Mwenyekiti wa CCM Wilaya |
| 10. | Mhe. Amri M. Mkalipa | __ | Katibu wa CCM Wilaya |
| 11. | Mhe. SP. Deogratius N. Mwanyasi | __ | Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya |
| 12. | Mhe. Maulidi H. Chambilila | __ | Katibu Mwenezi na Siasa CCM Wilaya |

**Wakuu wa Idara na Vitengo waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Pilly R. Kitwana | __ | Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Manispaa - Katibu |
| 2. | Ndg. Isaac Ashery | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu wa Manispaa |
| 3. | Ndg. Evance Y. Kutona | __ | Afisa Usafirishaji wa Manispaa |
| 4. | Eng. Juma Gwisu | __ | Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mijini wa Manispaa |
| 5. | CPA. Andrew Masanja | __ | Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa |
| 6. | Ndg. Raphael Kunambi | __ | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Manispaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Ndg. Jafari A. Makupula | __ | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi na Ununuzi wa Manispaa |
| 8. | Ndg. Dauson Jeremiah | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Hifadhi ya Mazingira wa Manispaa |
| 9. | Ndg. Samwel Subi | __ | Mkuu wa Kitengo cha Mazingira na Usafishaji wa Manispaa |
| 10. | Ndg. Festus Herman | __ | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji wa Manispaa |
| 11. | Ndg. Zena Cornel Lutego | __ | Kaimu Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa |
| 12. | Ndg. Safia Kingwahi | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa wa Manispaa |
| 13. | Ndg. Puppa Joseph | __ | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Manispaa |
| 14. | Ndg. Shaban Duru | __ | Afisa Rasilimali watu |
| 15. | Ndg. Elikarim S. Tyeah | __ | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa Manispaa |
| 16. | Ndg. Feliciana Katemana | __ | Mratibu wa TASAF wa Manispaa |
| 17. | Ndg. Upendo Elias | __ | Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa |
| 18. | Ndg. Fatuma Burhani | __ | Mhasibu wa Mapato |
| 19. | Ndg. Stephen N. Mkulia | __ | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi wa Manispaa |
| 20. | Dr. Charles R. Mkombachepa | __ | Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Manispaa |
| 21. | Ndg. Adam T. Shayo | __ | Mthibiti Ubora wa Shule Wilaya |
| 22. | Ndg. Faraja Maduhu | __ | Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii wa Manispaa |
| 23. | Ndg. Alatutosia Y. Sanga | __ | Afisa Masoko wa Manispaa |
| 24. | Ndg. Emeline E. Kihunrwa | __ | Afisa Mipangomiji wa Manispaa |
| 25. | Ndg. Michael Waluse | __ | Afisa Kilimo |
| 26. | Ndg. Norbert Bilaba | __ | Afisa Afya wa Manispaa |
| 27. | Ndg. Lilian Henerico | __ | Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Manispaa |

**Watendaji wa Kata waliohudhuria:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Baraka Lemaha | __ | Mtendaji wa Kata ya Mindu |
| 2. | Ndg. Amina Alphonce Liwongwe | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kauzeni |
| 3. | Ndg. Mariam Khalid Ngoda | __ | Mtendaji wa Kata ya Uwanja wa Taifa |
| 4. | Ndg. Laurent Masanja | __ | Mtendaji wa Kata ya Tungi |
| 5. | Ndg. Maria J. Shine | __ | Mtendaji wa Kata ya Kingo |
| 6. | Ndg. Ally Nassoro | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Mji Mkuu |
| 7. | Ndg. Andrew E. Luka | __ | Mtendaji wa Kata ya Mji Mpya |
| 8. | Ndg. Tatu H. Ally | __ | Mtendaji wa Kata ya Kihonda |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Ndg. Justa Medard | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kilakala |
| 10. | Adv. Masanja M. Nkinga | __ | Mtendaji wa Kata ya Luhungo |
| 11. | Ndg. Ibrahim Rashid Nguya | __ | Mtendaji wa Kata ya Kingolwira |
| 12. | Ndg. Mariam S. Rajabu | __ | Mtendaji wa Kata ya Lukobe |
| 13. | Ndg. Neema Peter Mang'ati | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Mwembesongo |
| 14. | Ndg. Yohana Obedi | __ | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Mlimani |
| 15. | Ndg. Witness Matowo | __ | Mtendaji wa Kata ya Kihonda Magorofani |
| 16. | Ndg. Hamisi Ally Ismail | __ | Mtendaji wa Kata ya Mkundi |
| 17. | Ndg. Josepher B. Kisaka | __ | Mtendaji wa Kata ya Magadu |
| 18. | Ndg. Prisca Mawallah | __ | Mtendaji wa Kata ya Boma |
| 19. | Ndg. Helena W. Mgallah | __ | Mtendaji wa Kata ya Bigwa |
| 20. | Ndg. Amina Said Mhina | __ | Mtendaji wa Kata ya Mafiga |
| 21. | Ndg. Lilian P. Kagoma | __ | Mtendaji wa Kata ya Sultan Area |
| 22. | Ndg. Sekela Kajigili | __ | Mtendaji wa Kata ya Mazimbu |
| 23. | Ndg. Merina C. Singano | __ | Mtendaji wa Kata ya Kichangani |
| 24. | Ndg. Aziza Omari | __ | Mtendaji wa Kata ya Kiwanja cha Ndege |
| 25. | Ndg. Fatma H. Mkwenda | __ | Mtendaji wa Kata ya Sabasaba |
| 26. | Ndg. Sada Said Mpina | __ | Mtendaji wa Kata ya Mbuyuni |
| 27. | Ndg. Mwajabu R. Hassani | __ | Mtendaji wa Kata ya Mafisa |
| 28. | Ndg. Christina Ngonyani | __ | Mtendaji wa Kata ya Mzinga |
| 29. | Ndg. Rajabu S. Wanyamale | __ | Mtendaji wa Kata ya Chamwino |

**Sekretarieti:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Daudi A. Kibwana | __ | Katibu wa Mikutano |
| 2. | Ndg. Deogratias Butabile | __ | Katibu wa Mikutano |
| 3. | Ndg. Theresia Mbena | __ | Katibu wa Mikutano |
| 4. | Ndg. Jimmy Katabaruki | __ | Katibu wa Mikutano |
| 5. | Ndg. Lilian Lemunge | __ | Katibu wa Mikutano |

HMM/BM/27/2022/2023 Kufungua mkutano

Baada ya akidi ya Wajumbe kutimia, Katibu alimkaribisha Mstahiki Meya ili afungue mkutano.

Mstahiki Meya (Mwenyekiti) aliwaongoza Wajumbe na watu wote waliohudhuria kuimba wimbo wa Taifa na alisoma dua ya kuiombea Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe, Viongozi wote na Wananchi kisha alifungua mkutano saa 5:25 asubuhi.

Baada ya kufungua mkutano Mstahiki Meya aliwakaribisha Viongozi walioalikwa kutoa salaam za Serikali kama ifuatavyo:-

**Salaam za Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro**

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani na Wataalam wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kazi nzuri wanayofanya. Alieleza kuwa hii ni mara yake ya kwanza kukutana na Wajumbe wa Baraza Madiwani la Manispaa ya Morogoro.

Alifafanua kuwa katika utendaji wake wa kazi wa kila siku amegundua umuhimu wa Waheshimiwa Madiwani katika kuiletea maendeleo Manispaa ya Morogoro kwa kuwa wao ndiyo wapangaji wa bajeti ya maendeleo ya Manispaa, wapangaji na wasimamizi wa matumizi ya fedha za Manispaa na wafuatiliaji wa fedha za maendeleo.

Ili kufanikisha yote hayo aliwasisitiza Wajumbe wa Baraza la Madiwani kutoa kipaumbele kusimamia hali ya ulinzi na usalama katika Kata zao na Manispaa kwa ujumla. Pia aliwasisitiza Waheshimiwa Madiwani waache tabia ya ubinafsi pindi Serikali ikileta fedha za miradi ya maendeleo ili kusiwe na mvutano wa mahala pa kujenga mradi kwani mradi huo ni kwa manufaa ya Wananchi wa Manispaa ya Morogoro.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana Manispaa ya Morogoro alitaja baadhi ya changamoto zinazoikabili Halmashauri kama ifuatavyo:-

**Kuhusu ukusanyaji mapato**

Katika kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022 Manispaa ya Morogoro ilionekana ndiyo ya mwisho katika ukusanyaji wa mapato kimkoa kwa kukusanya asilimia 24 wakati Halmashauri nyingine zimefikisha zaidi ya asilimia 50 kwa kipindi hicho.

**Kutokupelekwa kwa wakati fedha Benki**

Aliisisitiza Menejimenti kuhakikisha kuwa fedha zote za mapato zinazokusanywa zinapelekwa benki kwa wakati.

**Kuhusu upelekaji wa fedha za maendeleo asilimia 60 ya bajeti ya Halmashauri**.

Aliisisitiza Menejimenti kupeleka fedha za maendeleo asilimia 60 ya bajeti iliyoidhinishwa na Serikali.

**Kuhusu Wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo**

Aliwasihi Wananchi wawe wanashiriki kwa hali na mali katika shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na Halmashauri.

**Kuhusu mikopo ya mfuko wa maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

Halmashauri iendelee kutoa mikopo kwenye mfuko huo kwa kutumia asilimia 10 ya makusanyo yanayokusanywa. Alishauri changamoto zinazojitokeza zijadiliwe kwenye vikao vya Kamati za kudumu na kupata ufumbuzi.

**Salaam za Mwenyekiti wa CCM Wilaya**

Mwenyekiti wa CCM Wilaya aliunga mkono hoja zote zilizotolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro kwa utekelezaji.

**Salaam za Mkuu wa Wilaya ya Morogoro**

Alianza kwa kumpongeza Mhe. Fikiri Juma - Mwenyekiti wa CCM Wilaya kwa kutetea na kushinda nafasi yake ya uenyekiti. Aidha aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani na Watendaji kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ufanisi.

Aliwaagiza kuendelea kusimamia matumizi ya fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa zinazoendelea kuletwa na Serikali Kuu.

**Kuhusu changamoto zinazowakabili Wananchi wa Manispaa ya Morogoro**

Alieleza changamoto zinazowakabili Wananchi wa Manispaa ya Morogoro kama ifuatavyo:-

**Kuhusu uhaba wa maji**

Alieleza kuwa changamoto hiyo inatokanana mito kukauka hivyo aliwaagiza wananchi walinde maji machache yanayopatikana. Aliwaomba wenye uwezo wa kuchimba visima vya maji wachimbe na kuwasaidia watu wengine

**Kuhusu kukatika kwa umeme**

Alieleza kuwa kufuatia kulipuka kwa transfoma ya kupozea umeme katika kituo kikuu cha Msamvu Morogoro kumesababisha mgawo mkubwa wa umeme katika Mkoa wa Morogoro hivyo aliwasihi Wananchi waendelee kuwa na subira wakati jitihada za kuitengeneza zikiendelea. Aidha umeme unaotumika kwa sasa unapatikana kutoka Mikoa ya jirani.

**Kuhusu ubovu wa barabara**
Alieleza kuwa TARURA Wilaya inaendelea kutatua changamoto ya ubovu wa barabara.

**Kuhusu mradi wa reli ya Mwendokasi**
Aliwaomba wananchi wa Kata ya Chamwino wasiwazuie Wataalamu wanaoendelea na kazi ya kuchimba mashimo ya kupitisha nguzo za umeme ili kupeleka kwenye kituo cha kuendeshea treni ya Mwendokazi kwani serikali inaendelea kushughulikia kuwalipa madai yao ya fidia.

**Kuhusu usafi wa mazingira**
Aliwasisiza Wataalam na Wananchi kwa ujumla kwa kila Kata kufanya usafi kwenye maeneo yao kila siku ya Jumamosi.

**Kuhusu magari kuingia stendi ya Mafiga**
Alieleza kuwa wenye Daladala wako tayari kuingia katika stendi hiyo na kulipa mapato. Alimsisita mkusanyaji mapato mwenye mashine ya PoS awe anawahi saa 12:00 asubuhi kukusanya mapato.

Aliwaagiza Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Halmashauri, Viongozi wa Wilaya na wenye Daladala wiki ijayo wakutane ili kuweka sawa jambo hili. Aidha mtumishi akishindwa kutimiza wajibu wake katika kukusanya mapato achukuliwe hatua za kinidhamu.

HMM/BM/28/2022/2023 Kuridhia agenda za mkutano

Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo:-

1) Kufungua Mkutano
2) Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.
3) Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani:-
   - Tarehe 12/08/2022 (Taarifa za Kata)
   - Tarehe 15/08/2022 (Kawaida)
   - Tarehe 27/9/2022 (Kupitisha taarifa ya Hesabu za mwisho za Halmashauri).
4) Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 12/08/2022 (Taarifa za Kata) na tarehe 15/08/2022 (Kawaida).
5) Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo:-
   5.1 Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.

5.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.
5.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.
5.4 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.

7) Taarifa ya Kamati ya Bodi ya Ajira
8) Maombi ya kufuta madeni ya mishahara ya Watumishi waliolipwa mishahara kimakosa baada ya kustaafu utumishi wa Umma jumla ya **Tshs. 177,234,656.00**.
9) Mpango wa Mafunzo kwa Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.
10) Kuwasilisha muhtasari wa mrejesho wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2022/2023.
11) Taarifa ya mapokezi ya fedha **Tshs. 1,620,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 ya shule za Sekondari za Manispaa ya Morogoro
12) Taarifa ya kiutumishi
13) Kufunga Mkutano.

HMM/BM/29/2022/2023 Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.

**1.0 Kuhusu maombi ya matengenezo ya barabara ya zamani ya Iringa inayohudumia Kata nne za Magadu, Mzinga, Kauzeni na Luhungo:-**

Mjumbe mmoja alieleza kuwa barabara ya zamani ya Iringa (Old Iringa Road) inahudumia Kata ya Magadu, Mzinga, Kauzeni na Luhungo ni mbovu na aliiomba TARURA Wilaya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Majibu**

Ilielezwa kuwa swali hilo linahusu Taasisi nyingine ya TARURA, muhusika amealikwa lakini ana udhuru kwa hiyo majibu yatatolewa na TARURA Wilaya.

**2.0 Kuhusu Taarifa ya kukamilika ujenzi wa Soko la Kilakala:-**

Mjumbe alitoa taarifa kuwa Soko la Kilakala limekamilika japokuwa kuna changamoto ya umeme, maji, kusawazisha eneo la ulinzi. Mjumbe alitaka kujua ni lini changamoto hizo zitatatuliwa ili Halmashauri iweze kukusanya mapato na kuhudumia Wananchi.

**Majibu**

Mkurugenzi wa Manispaa alichukua changamoto zilizoainishwa hapo juu kwa ajili ya kuzifanyia kazi.

**3.0 Kuhusu tuhuma za mapato ya Halmashauri kuwa chini ya asilimia 25 kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba 2022 na kuwa ya mwisho Kimkoa:-**

Mjumbe alitaka kujua kuhusu tuhuma za mapato ya Halmashauri kuwa chini ya asilimia 25 kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 (Julai – Septemba, 2022) zimesababishwa na nini.

**Ufafanuzi:-**

Ilielezwa kuwa makisio ya mapato ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yapo juu **Tshs. 12,000,000,000.00** ukilinganisha na makisio ya Halmashauri zingine mfano Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi makisio yake ya mapato ni ni **Tshs. 3,000,000,000.00** kwa mwaka. Pili kuna mradi wa upimaji viwanja bado haujakamilika kuweza kuuza viwanja. Aidha Halmashauri inaendelea kutekeleza miradi yenye thamani kubwa ya fedha kulinganisha na Halmashauri zingine za Mkoa wa Morogoro.

Menejimenti ilifafanua kuwa uuzwaji wa viwanja utakamilika mwishoni mwa robo ya pili ya Oktoba – Desemba, 2022 na viwanja vitaanza kuuzwa na mapato yataongezeka.

**4.0 Kuhusu umaliziaji wa ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Mindu:-**

Mjumbe alitaka kujua ni lini Menejimenti itamalizia ujenzi wa ofisi ya Kata ya Mindu ili Watumishi waweze kuhamia.

**Majibu**

Mkurugenzi wa Manispaa alifafanua kuwa Menejimenti itatenga fedha kwenye bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2023/2024 sanjari na kuzitengea Kata nyingine zenye changamoto ya ofisi.

**5.0 Kuhusu mapendekezo ya kujenga chumba cha upasuaji katika Kituo cha Afya Mafiga:-**

Mjumbe aliuliza ni lini Halmashauri itajenga chumba cha upasuaji katika Kituo cha Afya Mafiga.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ina mpango wa kujenga vyumba vya upasuaji katika vituo vya Afya Mafiga na Sabasaba hivyo itatekelezwa.

**6.0 Kuhusu mabasi yanayoegeshwa nje ya stendi ya mabasi Msamvu na kupeleka abiria Hotelini kula na kupoteza mapato.**

Mjumbe alieleza kuwa yapo mabasi ya abiria yanaegeshwa hotelini nje ya stendi ya mabasi Msamvu kupata chakula na hayaingii stendi hivyo kupoteza mapato. Aidha, ilielezwa kuwa eneo hilo siyo stendi hivyo wazuiwe.

**Majibu**

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro amelichukua suala hilo na aliahidi kulifanyia kazi kwa kuwa sehemu hiyo siyo rasmi.

| | |
|---|---|
| HMM/BM/30/2022/2023 Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 12/08/2022 (Taarifa za Kata), tarehe 15/08/2022 (Kawaida) na tarehe 27/9/2022 (Maalum - kupitisha taarifa ya Hesabu za mwisho za Halmashauri). | Mihtasari haikuwa na masahihisho hivyo ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbkumbu sahihi za mikutano. |

HMM/BM/31/2022/2023 Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 12/08/2022 (Taarifa za Kata) na tarehe 15/08/2022 (Kawaida).

**1.0 Kuhusu utaratibu wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji za Kata.**

**Azimio:-**

Mstahiki Meya aliagiza kwenye mkutano ujao upangwe utaratibu kwa Waheshimiwa Madiwani watakaowasilisha taarifa za utekelezaji za Kata kwa zamu.

**Utekelezaji**

Agizo limezingatiwa. Utaratibu wa kuwasilisha taarifa kila Kata kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kila Kata umepangwa kama ifuatavyo:-

| NA | KATA | KIPINDI HUSIKA | TAREHE YA MKUTANO |
|---|---|---|---|
| 1 | Sabasaba | **Robo ya kwanza** Julai – Septemba 2022 | 25/10/2022 |
| | Mindu | | |
| | Mafisa | | |
| 2 | Mlimani | **Robo ya pili** Oktoba – Desemba, 2022 | 23/01/2023 |
| | Kauzeni | | |
| | Mwembesongo | | |
| 3 | Kihonda | **Robo ya tatu** Januari – Machi, 2023 | 24/04/2023 |
| | Kihonda Maghorofani | | |
| | Sultan Area | | |
| 4 | Mzinga | **Robo ya nne** Aprili – Juni, 2023 | Mwezi Julai, 2023 |
| | Mjimpya | | |
| | Boma | | |

Baraza lilipokea taarifa na kuipongeza Menejimenti kwa kuandaa ratiba.

**2.0 Kuhusu stendi ya Daladala Mafiga:**

**Azimio**

Wajumbe walitoa muda wa siku 30 kuanzia tarehe 16/08/2022 magari yote ya kusafirisha abiria kwenda Wilayani yaanzie stendi ya Daladala Mafiga. Aidha, magari ya Daladala (Hiace) ziingie katika stendi ya Daladala ya Mafiga.

**Utekelezaji**

Agizo limezingatiwa. Mkurugenzi wa Manispaa ametoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ili kushirikisha Taasisi nyingine zenye mamlaka na suala la usafirishaji ambazo ni Jeshi la Polisi, Kikosii cha Usalama barabarani, LATRA na Manispaa ya Morogoro. Menejimenti inasubiri ushirkishwaji wa Taasisi hizo katika kutekeleza agizo hili.

**3.0 Kuhusu mikataba ya kuwapangisha Wafanyabiashara katika Stendi ya Daladala Mafiga.**

**Azimio**

Baraza la Madiwani lilikasimu madaraka kwa Kamati ya Fedha na Uongozi kushughulikia mikataba ya kuwapangisha Wafanyabiashara waliopanga kwenye Stendi ya Daladala Mafiga kujua kiasi cha kodi ya pango watakayotozwa kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, Kamati hiyo pia ishughulikie sehemu ya kudumu watakayohamishiwa baada ya kipindi cha mwaka mmoja na kuwasilisha taarifa kwenye mkutano ujao.

**Utekelezaji**

**Kuhusu eneo la kudumu la kuwahamishia Wafanyabiashara**

Ilielezwa kuwa kwa kuwa mradi huo unatekelezwa na wadau wawili ambao ni SUA na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro walioingia mkataba wa kuendeleza eneo hilo kwa ubia. Menejimenti iliwasilisha hoja hiyo kwa wabia SUA na bado inaendelea kujadiliwa ili kupata eneo la kudumu la kuwahamishia Wafanyabiashara baada ya mwaka mmoja uliotolewa na Baraza la Madiwani.

**Kuhusu uandaaji wa mikataba**.

Ilielezwa kuwa Wafanyabiashara wanadai kiwango cha kuwapangisha kwa mita moja ya mraba kwa **Tshs. 500.00** ni kikubwa, hivyo mazungumzo kati ya Halmashauri na wafanyabiashara bado yanaendelea ili kukubaliana kiwango sahihi cha kutoza, pindi makubaliano yatakapoafikiwa taarifa itawasilishwa Kamati ya Fedha na Uongozi.

**Maamuzi na maagizo**

Baraza la Madiwani lilitoa muda wa siku saba (wiki moja) kuanzia tarehe 28/10/2022 Wafanyabiashara wa stendi ya Daladala Mafiga wasaini mikataba ya kupangishwa maeneo kwa mita moja ya mraba **Tshs. 500.00** na waanze kulipa.

HMM/BM/32/2022/2023 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo.

**1.0 Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.**

Taarifa iliwasilishwa, iliungwa mkono, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**2.0 Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.**

Taarifa iliwasilishwa, iliungwa mkono, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**Mjadala**

Wajumbe waliielekeza Menejimenti itenge fedha za kutosha kwenye bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2023/2024 ili kutatua changamoto zilizoainishwa kwenye ukurasa wa 52 Namba 2.2 kama vile kuchonga samani za shule, kusambaza vitabu vya wanafunzi na kuboresha miundombinu ya shule kama vile vyoo.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa upo mkakati mkubwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kutenga fedha za kutosha kutatua changamoto zilizotajwa kwenye Sekta ya elimu.

**Kuhusu ununuzi wa vishikwambi**

Baraza lilisisitiza vishikwambi vinunuliwe mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2022. Menejimenti ilipokea taarifa hiyo na ilifafanua kuwa vishikwambi vitanunuliwa na pia kutakuwa na mafunzo ya namna ya kuvitumia na kuvitunza.

**3.0 Taarifa ya Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.**

Taarifa iliwasilishwa, iliungwa mkono, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**Mjadala**

**Kuhusu Kikundi cha usafi wa mazingira Kata ya Mindu kushindwa kufanya kazi.**

Ilielezwa kuwa mkataba utavunjwa na kusainiwa na Kikundi cha usafi wa mazingira cha Kata kuhusu milima mingi kuungua moto.

Wajumbe wa Baraza la Madiwani lilielekezwa kuwa Wananchi wapewe elimu waache tabia za kuwasha moto milima ili kulinda mazingira.

**4.0 Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023**

Taarifa iliwasilishwa,ilipokelewa, iliungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Madiwani waliiridhia.

HMM/BM/33/ 2022/2023 Taarifa ya Kamati ya Bodi ya Ajira.

Ilielezwa kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro ilipokea kibali cha ajira chenye **Kumb. Na. FA.97/228/01/9** cha tarehe 13/5/2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuajiri nafasi ya Udereva nafasi **3** na Watendaji wa Mtaa nafasi **11**.

Bodi ya Ajira kupitia vikao vyake vya tarehe 31/08/2022 na tarehe 2/02/2022 vilifanya mchakato wa kuajiri ambapo katika nafasi ya udereva walioomba ni watu 499 baada ya mchujo walioitwa kwenye usaili ni watu 186 waliofika kwenye usaili wa vitendo ni 20. Baada ya usaili wa vitendo watu 8 walipatikana na kufanyiwa usaili wa mahojiano ya ana kwa ana na kupata madereva 3 ambao ni:-

1. Frank Kassim Nguta.
2. Heri M. Mtanga
3. Juma Sabihi Hakika.

Katika nafasi ya Utendaji wa Mtaa walioomba ni watu 3,741 baada ya mchujo walioitwa kwenye usaili ni watu 1,673 waliofika kwenye usaili ni watu 291, kati yao watu 40 waliitwa kwenye usaili wa mahojiano ya ana kwa ana. Baada ya usaili huo waliopata nafasi hiyo ya Utendaji wa Mtaa ni kama ifuatavyo:-

1. Godlisten Nnko.
2. Maurus Christian Nduguru.
3. Grace Damson Badi.
4. Joseph Ernest.
5. Amati Paul Amati.
6. Maritha Philipo Marcel.
7. Sheila Yasin Mningo.
8. Shamimu Seif Abdallah.
9. Herieth F. Timbuka
10. Irene Mazsmo Msalichuma.
11. Paulina Fillingson Kayuni.

Tayari Watumishi hawa wapo kwenye vituo vyao vya kazi na wanaendelea na majukumu yao.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuiridhia.

HMM/BM/34/2022/2023 Maombi ya kufuta madeni ya mishahara ya Watumishi waliolipwa mishahara kimakosa baada ya kustaafu utumishi wa Umma jumla ya **Tshs. 177,234,656.00.**

Iliwasilishwa orodha ya Watumishi waliolipwa mishahara kimakosa baada ya kustaafu utumishi wa wa umma kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2014 – 2020 ili kuweza kuiondoa hoja hiyo. Aidha, juhudi za kuwapata Wastaafu zimeshindikana kwani wamestaafu utumishi wa umma muda mrefu na hawapatikani kwa mawasiliano ya kimtandao. Hoja ilikuwa **Tshs. 271,015,000.00** na imepungua hadi **Tshs. 93,780,344.00** Wastaafu waliobaki ni **Tshs. 177,234,656.00.**

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuiridhia.

HMM/BM/35/2022/2023 Mpango wa mafunzo kwa Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Taarifa iliwasilishwa kama ifuatavyo:-
Menejimenti iliwasilisha mpango wa mafunzo kwa Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ilielezwa kuwa Watumishi 179 wameomba nafasi ya kwenda masomoni kujiendeleza kielimu na kupewa ruhusa kupitia kwenye Divisheni na Vitengo vyao kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | DIVISHENI | IDADI |
|---|---|---|
| 1 | Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi | 11 |
| 2 | Divisheni ya Elimu Sekondari | 30 |
| 3 | Divisheni ya Elimu ya Awali na Elimu Msingi | 83 |
| 4 | Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe | 32 |
| 5 | Divisheni ya Rasilimali Watu na Utawala | 18 |
| 6 | Divisheni ya Mipango na Uratibu | 2 |
| 7 | Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira | 2 |
| 8 | Kitengo cha Fedha na Uhasibu | 1 |
| | **JUMLA** | **179** |

Watumishi hao wote watajigharamia wenyewe mafunzo yao.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuiridhia kwa utekelezaji.

| | |
|---|---|
| HMM/BM/36/ 2022/2023 Kuwasilisha muhtasari wa mrejesho wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2022/2023. | Ilielezwa kuwa Halmashauri kupitia mkutano wake wa Baraza la Madiwani wa tarehe 29/02/2022 ulipitisha makadirio ya fedha **Tshs. 84,978,512,600.00** na kuwasilishwa Hazina kwa ajili ya uchambuzi na kupokea maelekezo ya kisera na miongozo mingine ya kiutendaji kwa lengo la kutekeleza ilani ya Chama Tawala cha CCM.<br><br>Baada ya kupitiwa kwa kina kwa kufuata viwango vipya vya ukomo (celling) Hazina iliidhinisha jumla ya **Tshs. 84,561,722,000.00** hii ikiwa ni mjumuisho wa Bajeti ya mapato ya ndani, fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na miradi ya maendeleo kwa mchangauo ufuatao:-<br><br>**Mishahara Tshs. 61,640,104,000.00**<br>Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha **Tshs. 64,422,957,000.00** kiliombwa na Halmashauri na kiasi cha **Tshs. 61,640,104,000.00** kiliidhinishwa na Hazina kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.<br><br>**Matumizi mengineyo Tshs. 1,152,173,000.00**<br>Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri iliomba **Tshs. 1,228,006,000.00** lakini Hazina iliidhinisha jumla ya **Tshs. 1,152,173,000.00** ili kugharamia matumizi mengineyo.<br><br>**Mapato ya ndani ya Halmashauri Tshs. 12,654,400,000.00**<br>Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ilijipangia kukusanya jumla ya **Tshs. 10,754,563,600.00** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato na kuzigawanya katika sekta mbalimbali ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kiutawala na miradi mbalimbali. Hata hivyo, Hazina/TAMISEMI iliidhinisha jumla ya **Tshs. 12,654,400,000.00** zikusanywe na Manispaa ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 23 ukilinganisha na makisio yaliyokuwa katika mwaka 2021/2022 baada ya kufanyiwa mapitio ambayo ni **Tshs. 10,255,736,199.95.**<br><br>**Miradi ya maendeleo (Ndani – Serikali Kuu) Tshs. 5,014,326,000.00**<br>Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri iliomba **Tshs. 2,707,846,000.00** lakini Hazina iliidhinisha jumla ya **Tshs. 5,014,326,000.00** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. |

**Miradi ya Maendeleo (Nje – Wahisani) Tshs. 4,100,719,000.00**
Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri iliomba **Tshs. 5,861,149,000.00** lakini Hazina iliidhinisha jumla ya **Tshs. 4,100,719,000.00** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Hivyo basi, katika mwaka huu wa fedha Manispaa itatekeleza miradi yenye thamani ya **Tshs. 14,904,034,000.00** ambapo fedha za ndani (Serikali kuu) ni **Tshs. 5,014,326,000.00** na za nje (Wahisani) **Tshs. 4,100,719,000.00.** Halmashauri kupitia fedha za mapato ya ndani (own source) ilitenga kutekeleza miradi yenye thamani ya **Tshs. 5,788,989,000.00.**

**Mapato**
Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imeidhinishiwa kukusanya jumla ya **Tshs. 84,561,722,000.00** kutokana na vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo:-

| Chanzo cha mapato | Mchangiaji | Makisio 2022/2023 |
|---|---|---|
| Vyanzo vya Halmashauri | Halmashauri | 12,654,400,000.00 |
| Ruzuku – Matumizi ya kawaida (OC) | Serikali Kuu | 1,152,173,000.00 |
| Ruzuku – Mishahara | Serikali Kuu | 61,640,104,000.00 |
| Ruzuku – Miradi ya Mendeleo | Serikali Kuu | 5,014,326,000.00 |
| Ruzuku – Miradi ya Mendeleo | Wahisani | 4,100,719,000.00 |
| **JUMLA** | | **84,561,722,000.00** |

**Matumizi**
Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imeidhinishiwa kutumia jumla ya **Tshs. 84,561,722,000.00** katika matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

| Chanzo cha mapato | Mchangiaji | Makisio 2022/2023 |
|---|---|---|
| **A. Vyanzo vya Halmashauri** | | |
| (i) Mishahara | Halmashauri | 47,542,000.00 |
| (ii) Matumizi ya kawaida | Halmashauri | 3,811,784,000.00 |
| (iii) Miradi ya Mendeleo | Halmashauri | 5,788,989,000.00 |
| (iv) Mapato Lindwa (Protected Fund) | Halmashauri | 3,006,085,000.00 |
| **JUMLA** | | **12,654,400,000.00** |

| | | |
|---|---|---|
| **B. Ruzuku** | | |
| (i) Mishahara | Serikali Kuu | 61,640,104,000.00 |
| (ii) Matumizi ya kawaida | Serikali Kuu | 1,152,173,000.00 |
| (iii) Ruzuku - Miradi ya Mendeleo | Serikali Kuu | 5,014,326,000.00 |
| (iv) Ruzuku – Miradi ya Maendeleo | Wahisani | 4,100,719,000.00 |
| **JUMLA** | | **71,907,322,000.00** |
| **JUMLA KUU** | | **84,561,722,000.00** |

**Muhtasari wa mrejesho wa bajeti ya mwaka 2022/2023 ikionesha tofauti kati ya bajeti iliyopita na Baraza la Madiwani la tarehe 29/02/2022 na bajeti iliyoidhinishwa na Hazina.**

| NA. | Kasma | Bajeti iliyopitishwa na Baraza la Madiwani la tarehe 22.02.2016 (Tshs) | Bajeti iliyoidhinishwa na Hazina (Tshs) | Kiasi kilichopungua/ongezeka (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| A | Mshahara | | 61,640,104,000.00 | (2,782,853,000.00) Upungufu huu ni kutokana na kufutwa kwa ajira mpya na promotion za watumishi. |
| B | Matumizi mengine | | 1,152,173,000.00 | (75,833,000.00) Upungufu huu ni wa fedha za capitation Msingi na Sekondari pamoja na Ruzuku ya Utawala(GPG) na Ruzuku ya Sekondari |
| C | Miradi ya maendeleo (L) | | 5,014,326,000.00 | Tshs. 2,306,480,000.00 ni ongezeko katika maeneo yafuatayo:- (a) Ujenzi wa Hospitali na vifaa vya Afya na Zahanati, (b) Mfuko wa Jimbo, (C) Ukarabati wa shule kongwe na ujenzi wa shule mpya 1, ukamilshaji wa madarasa na uzio wa mabweni ya watoto wenye mahitaji maalum |
| D | Miradi ya maendeleo (F) | | 4,100,719,000.00 | Tshs. 1,760,430,000.00 ni upungufu pamoja na baadhi ya miradi mipya kuongezeka kama vile boost, GAVI SEQUIP, Lishe Endelevu. |
| E | Mapato ya ndani | | 12,654,400,000.00 | (Tshs 2,398,663,800.00) ni ongezeko la asilimia 23 ukilinganisha na bajeti 2021/2022. Maaneo yaliyoongezewa bajeti ni uuzaji wa viwanja, leseni za biashara na ushuru wa huduma |
| | **JUMLA** | | **84,561,722,000.00** | |

Menejimenti iliwasilisha taarifa ya mrejesho wa Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa mwaka 2022/2023 ya **Tshs. 84,561,722,000.00** kama ilivyoidhinishwa na Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na marekebisho yake.
Wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo.

| | |
|---|---|
| HMM/BM/37/ 2022/2023 Taarifa ya mapokezi ya fedha **Tshs. 1,620,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 ya shule za Sekondari za Manispaa ya Morogoro. | Ilielezwa kuwa Manispaa ya Morogoro ilipokea kiasi cha **Tshs. 1,620,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **81** ya shule za Sekondari za Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kupokea Wanafunzi wa kidato cha kwanza, 2023.<br><br>**Mjadala na maamuzi**<br>Wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo. Aidha, walimpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta fedha hizo kwa maendeleo ya Wananchi wa Manispaa ya Morogoro. |
| HMM/BM/38/ 2022/2023 Taarifa ya Kiutumishi | Kabla ya kujadili agenda hii, Baraza la Madiwani lilijigeuza kama Kamati na taratibu za uendeshaji wa vikao vya Kamati za kudumu kwa mujibu wa Kanuni 37 na 38 ya kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro zilifuatwa.<br><br>Afisa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Manispaa aliwasilisha taarifa ya upekuzi wa Mhandisi Matogolo Juma Gwisu - Mhandisi Daraja la I ili aweze kuteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundombinu Vijijini na Mijini. Taarifa ya upekuzi ilionesha kuwa muhusika hana dosari zozote za kiusalama, kiutendaji wa kitabia hivyo anaweza kufikiriwa kuteuliwa kama ilivyopendekezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.<br><br>Aidha, Katibu Mkuu Utumishi aliridhia Mhandisi Matogolo Juma Gwisu akaimu na kulipwa posho ya kukaimu nafasi ya Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundombinu, Vijijini na Mijini kwa miezi sita (6) kuanzia tarehe 01 Agosti 2022 na kukamilisha utaratibu wa kujaza nafasi hiyo katika kipindi cha miezi sita (6). |

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Manispaa chini ya kifungu cha 6(1)(b) cha sheria ya Utumishi wa Umma sura ya 298 kikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 6(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Aya ya 12(b) ya taratibu za uendeshaji utumishi wa umma za mwaka 2003 aliagizwa aendelee na mchakato wa uteuzi na kutoa taarifa baada ya uteuzi kwa Katibu Mkuu Utumishi.

**Maamuzi**

Wajumbe wa Baraza la Madiwani walipokea taarifa hiyo na kuridhia Mhandisi Matogolo Juma Gwisu ateuliwe kuwa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundombinu Vijijini na Mijini. Mapendekezo yawasilishwe kwa Katibu Mkuu Utumishi kwa hatua zaidi.

| | |
|---|---|
| HMM/BM/39/ 2022/2023 Kufunga Mkutano | Kabla ya kufunga mkutano, Mstahiki Meya aliisisitiza Menejimenti kwa kushirikiana na Watendaji wa Kata na Mitaa kukusanya mapato ya Halmashauri. Aidha alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Morogoro kwa kutoa ushirikiano katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri. Aliwasisitiza Wafanyabiashara waliopanga kwenye maeneo ya stendi ya Daladala Mafiga kuingia mikataba na kulipa mapato kwa mujibu wa sheria. |

Aliwaomba Viongozi wa Wilaya na Mkoa kuendelea kutoa ushirikiano na Viongozi wa Manispaa ya Morogoro katika kukusanya mapato ili kuweza kufikia malengo yaliyopangwa kwenye bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Kuhusu magari yanayoegeshwa nje ya stendi ya Msamvu. Alieleza kuwa sehemu hiyo siyo rasmi na salama kwa ajili ya abiria kupata chakula hivyo yafuatiliwe yaingie stendi ya Msamvu.

Baada ya maagizo hayo Mstahiki Meya alifunga Mkutano saa 7:30 mchana.

Muhtasari umethibitishwa tarehe ……………………………………………………………

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| Mhe. Pascal M. Kihanga | Ndg. Ally H. Machela |
| MSTAHIKI MEYA | MKURUGENZI WA MANISPAA |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 27/10/2022**

| MUHT. NA | AZIMIO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| HMM/BM/31/2022/2023 Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 12/08/2022 (Taarifa za Kata) na tarehe 15/08/2022 (Kawaida). | **1.0 Kuhusu mikataba ya kuwapangisha Wafanyabiashara katika Stendi ya Daladala Mafiga.**<br>Baraza la Madiwani lilitoa muda wa siku saba (wiki moja) kuanzia tarehe 28/10/2022 Wafanyabiashara wa stendi ya Daladala Mafiga wasaini mikataba ya kupangishwa maeneo kwa mita moja ya mraba **Tshs. 500.00** na waanze kulipa. | Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi. | Agizo limezingatiwa. Menejimenti ilifanya mawasiliano na Mbia (SUA) kutaka maoni yao juu ya kupangisha eneo hilo kwa kiwango tajwa cha **Tshs. 500.00** kwa mita moja ya mraba. Kwa bahati nzuri Mbia (SUA) imeridhia na kukubaliana na maoni ya Baraza ya kuwasainisha mikataba wapangaji. Mikataba imeandaliwa na tayari wafanyabiashara wameanza kuchukua mikataba yao. |